

DHIA YA METHALI *KATIKA* UKUZAJI WA NIDHAMU BAINA YA W ANAJAMII KIJINI  
BUNGANDARO, WILA Y ANI RUBANDA NCHINI UGANDA

A TWINIRAMASIKO IVAN

17 / A/BAED/1089/F

TASNIFU YA UTAFITI ILIYOTOLE WA KW A LEN GO LA KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA KUHITIMU SHAHADA YA UALJMU KA TIKA  
CHUO KIKUU CHAKABALE.

JANUARI- 2021

## **DIBAJI**

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza dhima ya methali katika ukuzaji wa nidhamu baina ya wanajamii kijijini Bungandaro, wilayani Rubanda nchini Uganda. Dhima za methali katika ukuzaji wa nidhamu zilichunguzwa katika utafiti huu. Aidha utafiti huu umeziainisha methali katika makundi matatu makuu, yaani uainishaji huu hutegemea maana ya ndani pamoja na maana ya nje na walengwa wa methali husika. Vile vile, methali zimeainishwa kulingana na maudhui ya kirnsingi yanayowasilishwa ndani ya methali hiyo hiyo, pamoja na uainisho wa kimafunzo. Makundi hayo ni pamoja na: Methali za kukashifu tabia mbaya mionganoni mwa wanajamii, Methali za kuhimiza heshima kwa wazima mionganoni mwa wanajamii pamoja na Methali za kuleta amani mionganoni rnwa wanajamii. Basi, makundi haya yote hukuza na kutimiza swala la nidhamu baina ya wanajamii. Utafiti huu umeundwa na sura tano yaani sura ya kwanza, pili, tatu, nne na tano. Sura ya Kwanza imeshughulikia Utangulizi, Tatizo la utafiti, Malengo ya Utafiti, Upeo wa utafiti, Umuhimu wa Utafiti na Changamoto zilizoukabili utafiti huu. Sura ya Pili imeshughulikia Mapitio ya Kitaaluma na ya Kazi tangulizi ambapo imeelezea yaliyoandikwa kuhusu methali na jinsi zinavyoweza kukuza nidhamu baina ya wanajamii. Aidha, imeelezea yaliyoandikwa kuhusu makundi pamoja na uanisho wa methali katika hali au masuala tofauti tofauti. Kadhalika, sura ya pili imeelezea Pengo la Maarifa na Kiunzi cha utafiti wa awali pamoja na jinsi utafiti huu ulivyoziba kiunzi au pengo hilo. Sura ya Tatu imezungumzia Njia na Mbinu za Utafiti. Imezungumzia Utangulizi, Eneo la Utafiti, Sampuli ya Utafiti na Usampulishaji, Ukusanyaji wa Data, Uchambuzi wa Data na Yifaa vya Utafiti. Sura ya Nne imeeleza juu ya Uwasilishaji na Uchambuzi wa data, ambapo imeelezea aina za teknolojia ambazo huwa na dhima katika ukuzaji wa nidhamu. Sura ya tano imeeleza juu ya Muhtasari wa Utafiti na Mapendekezo.